


# ATD Dunia ya Nne Tanzania
# Marejeo ya 2014

**ATD Dunia ya Nne**
Imesajiliwa kwa namba 003447 chini ya sheria ya Asasi zisizo za kiserikali ya mwaka 2002
S.L.P. 61786, Dar es Salaam – Tanzania
atd.tanzania@gmail.com
Tovuti ya Kiingereza: www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html
Tovuti ya Kiswahili: www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html

## Tupo Pamoja! (We are together!)

Mwaka 2014,bega  kwa bega pamoja na akinamama, akinababa, watoto, marafiki na jamii zinazoishi katika umaskini uliokithiri, Hivi ndio wanachama wa ATD Dunia ya Nne wamekua wakielezeana.

Shukrani kwa juhudi zote, tulizozijenga na nguvu zetu kwa ushirikiano uliotuwezesha kupambana na hali ngumu ya maisha ya kila siku.

Mwaka huu wa 2014 marejeo ya mwaka, tungependa kuonyesha juhudi na kujivunia kwa wale wote ambao, mbali na matatizo na changamoto walizonazo, walijitolea na watu wengine kuziwezesha familia na jamii katika kupambana na umaskini uliokithiri





# Wote kwa pamoja katika utu (ATD) kwa kirefu

"**Wote kwa pamoja**" inamaana ya muungano wa harakati, pia ni muhimu kuungana na juhudi za kila mmoja katika kufikia lengo la.

**"Utu"** ambayo inawakilisha harakati za ATD. Wanachama wa ATD amabao wanaishi katika umaskini uliokithiri na marafiki wanaelezea kwamba heshima inamaana ya thamani ya kila binadamu,hivyo basi kila mtu anapaswa kuheshimiwa. Heshima ni kiini cha Ubinadamu;kila mtu anaheshima.lakini katika kesi nyingi binadamu hawaheshimiwi. .

ATD Dunia ya Nne taasisi ya kimataifa ya harakati iliyoanzishwa Ufaransa mwaka 1957. Hivi sasa ina matawi katika nchi zaidi ya 30. Tulianza kufanya kazi Tanzania mnamo mwaka 1999 katika sehemu tatu za Dar es Salaam: Tandale, Tegeta (Kunduchi na Boko) na soko la Samaki la Magogoni.

Watu wanaoishi katika Umasikini uliokithiri wapo katikati mwa harakati zetu, tunashiriki kikamilifu katika kutatua Umasikini uliokithili, kwa pamoja tunasimamia haki za wote, tunatengeneza ufahamu na kwa watu na kushawishi sheria za umma



# Changamoto na mafanikio ya ATD Tanzania, mwaka 2014

Mara kwa mara tukiangalia miaka ya nyuma, tunafikiria matatizo tuliopitia. Tunakumbuka wanachama wetu wa karibu wa ATD waliofariki Dunia, na Vifo vya kusikitisha vya watoto wadogo.

Kwa juhudi zote zinazofanywa na watu wanaoishi na Umasikini kila siku, kusafisha Samaki, kutembea maili kadhaa ili kupata pesa kidogo, kufua nguo, kuvunja mawe, watu wengi hutuambia kwamba hakuna matumaini ya maisha kwetu.

***Mama mmoja alisema,***
***“nafikiria nini nitafanya kwa watoto wangu wakubwa wawili, Nimeshindwa kukabiliana na swala hilo.***
***Itabidi unitafutie mtu wa kumkabidhi watoto wangu wakubwa, ili mimi nibaki na mdogo.”***

Mama huyo hakuondoka, alisubili kama watu wote wanaoishi katika Umasikini uliopitiliza ambao hawakubali kukata Tamaa ya maisha yao. Watu wanaoishi katika Umasikini mara nyingi huongelea maisha kama ni *“mapambano”.*

Wanachama wa ATD wanajua kwamba hapatakua na ushindi katika mapambano hayo kwasababu ya kutengwa .
Umoja ni silaha kubwa katika Vita dhidi ya Umasikini uliopitiliza.

Katika mwaka 2014 sisi wanachama wa ATD, tumeweka ahadi upya katika mapambano dhidi ya Umasikini uliopitiliza kupitia vitendo na maneno, kupitia uelewa wetu na kupitia umoja wetu.



*"Namna gani ATD itatusaidia Kusonga mbele mkono kwa mkono? Kuonyesha kwamba tunakataa Umasikini uliopitiliza? Nataka kuondoa Umasikini uliopitiliza, kutoona watu wakiishi katika umasikini uliopitiliza, kwasababu swala hilo hutuumiza sana."*

**Mama Sele**

## Mkutano katika Maktaba ya Taifa Matarajio yetu ya kawaida

Januari, wanachama wa ATD walikutana katika maktaba kuu ya taifa ambapo ulifanyika uzinduzi wa Matarajio ya ATD Dunia ya nne 2014 - 2017. Katika makundi madogo wanachama wa ATD walifanya kazi kwa pamoja ili kujua kazi zao ili kufikia matarajio yao.

Vilevile mkutano huu ulikua ni nafasi ya kupata habari kutoka kwa waratibu wa ATD wa kanda ya Africa ambao wamekuja kutembea Dar es Salaam. Mkutano uliisha kwa kuwatakia safari njema ya kwenda kutembelea wanachama wengine wa ATD waliopo Rwanda na Jamuhuri ya muungano ya Congo.



## *Tukio Maalum*

***"Nje ya Tanzania nimejifunza kwamba watu wanaishi kwa amani hata katika nchi isiyo na amani."***
***Shabani***

## Kutembelea marafiki wa ATD waliopo Rwanda na JM Congo

Mapambano ya Umasikini uliokithiri ni changamoto iliyopo dunia nzima. ATD ni harakati za kimataifa, hutengeneza uhusiano wa  watu ili kutokomeza Umasikini uliokithiri.

Mwaka 2014, Wajumbe kutoka Tanzania walienda kutembelea wanachama wa ATD wa Rwanda na JM Congo (Shabani, Bibi Teddy na Hamisi).

Ilikua ni nafasi ya kukutana na wengine, kutengeneza urafiki, kugundua maisha ya watu wengine. Watu hugundua kwamba hawapo peke yao; Tanzania, Rwanda na JM Congo, watu wanapigania kitu kimoja.

Mjumbe wa Tanzania alishiriki kwa pamoja na watoto wa JM Congo katika kazi mbalimbali, kuimba, kucheza ambapo walijifunza kutoka kwa watoto wa maktaba ya mtaani ya Tandale.

Waligundua nia za watu, kwa kupitia mtandao mkubwa unaojumuishwa na makundi yanayotegemea umri wao. Mshikamano mkubwa unakuwepo kati ya wanachama: watoto wanasaidia kurekebisha Nyumba zao, watu wakubwa wanashiriki katika Maktaba ya Mtaani.......

Kugundua njia ya namna gani Jamii itajiandaa kama kundi, ***"...ilikua ni kitu kigeni katika maisha yangu." (Bibi Teddy)***


Potatoes
bananas
Protein Foods:
What are protein foods?
Protein foods are foods

# *Upatikanaji wa Haki*

***"Mtoto wangu wa kike hajaenda shuleni kwa muda wa miaka 3, lakini hatua kwa hatua, kwa kukutana na ATD, Tumefanikiwa kumrudisha shuleni."***
***Mama Meresiana.***

## Elimu kwa wote

***"Ilinilazimu kuanza shule tena baada ya kuhama, niliwekwa katika darasa la Memkwa pamoja na mdogo wangu wa kike ambapo nilikaa kwa kipindi kirefu. Niliacha kwenda shule kwasababu nilichoka kua darasa moja na watoto ambao walikua ni nusu ya umri wangu"***

Hiyo ni moja ya mifano ya kwanini watoto wanaoishi katika Umasikini uliopitiliza wanashindwa kwenda Shuleni. Mwaka 2014, ATD ilizindua Mswaada kabambe, Elimu kwa wote. Lengo lake, ni kuonyesha pindi Familia zilizopo katika Umasikini uliopitiliza wanahusika katika kila hatua ya watoto wao katika swala la Elimu, watoto wote watafanikiwa kuanza na kumaliza Elimu ya msingi.

***Hatua ya kwanza ya mradi huu ni utafiti shirikishi,*** kugundua juhudi na changamoto ambazo familia na walimu hufanya ili kufanya watoto waende Shule.

Kikundi cha utafiti chenye mchanganyiko wa wanachama mbalimbali wa ATD kilitengenezwa ili kutengeneza mpango, kuwezesha na kufanya zoezi la utafiti, ambalo litafanyakazi hadi 2015.


RAMBLER

# Watoto

*“**Inatoa changamoto ya kusoma na kushirikiana na wengine, kwa mfano wangu mdogo kabla hajahudhuria maktaba ya mtaani, hakutaka kusoma wala kufanya kitu chochote, lakini sasa anapenda kusoma na kuchukua vitabu mwenyewe, anahadithiana hadithi na wenzake, sasa hivi amekua mpole.”***

***Mama Feisali***

## Maktaba ya Mtaani

Maktaba ya mtaa ni sehemu ya kuchangia na kufurahia kwa pamoja kwa kutumia vitabu vya hadithi, kutengeneza urafiki na kutokujiona upo peke yako. Maktaba ya mtaa inasaidia watoto kukaa na watoto wenzao katika jamii yao. Wanajifunza namna ya kuishi kwa pamoja, kuheshimiana, kushirikiana kwa pamoja kama vile katika kuchora pale wanapoazimana kalamu na vifaa vingine.

Kila jumatano jioni kabla ya Maktaba ya Mtaa wa Tandale, tunatembelea Majumbani ili kuwakumbusha watoto na Familia. Chini ya mti tunaanza kuimba kwa pamoja, kucheza, na tunaanzisha michezo mbalimbali. Kisha tunakaa kwa pamoja na kujikumbusha sheria muhimu na kusoma hadithi, muda mwingine watoto wakubwa husoma Hadithi. Kisha unafika muda wa Ubunifu kama vile kujifunza namna ya kuchora wanyama, kupaka rangi au michezo mingine.

***“Maktaba ya Mtaa ni kama siku ya Familia,inatoa faida kwa watoto ” -***
***Bibi Teddy***

***Vile vile kupitia Hadithi watoto husoma, hugundua na huchunguza vitu vipya na mawazo ambayo hayapo katika mazingira yao. Hii ni nafasi kwa watoto ambao hubaguliwa kukubaliana na kuhisi usawa baina yao. Usomaji wa vitabu na hadithi hufanya watoto wafurahie kusoma. Ni sehemu ambayo huwapa watoto Uhuru, panakua hapana ukali kama shuleni, hii ni njia nzuri ya kusoma ambayo huwaandaa watoto kwaajili ya Shule.***



## *Upatikanaji wa Haki*

# Cheti cha kuzaliwa

***"Kabla tulijua kwamba upatikanaji wa cheti cha kuzaliwa ni jambo lisilowezekana, lakini ATD ilibadilimawazo yetu."* Mama Mkude**

***Mwaka 2014, tuliendelea na Mradi wetu wa vyeti vya kuzaliwa. Kila wiki sehemu ya Tandale au Tegeta, wanachama wa ATD Venance, Shabani na Baba Meresiana walikua na kazi ya kusaidia Familia zilizopo katika Umasikini uliopitiliza kupata vyeti vya kuzaliwa.***

Wazazi wa Tandale huhimizana kuondokana na changamoto na kutafuta makaratasi muhimu pindi timu ilipotembelea Nyumba nyingine.

Pamoja tumefanikiwa kusajili watoto 176.

***Usajili wa kuzaliwa ni muhimu sana kwasababu inamaanisha kwamba mtu Fulani 'kisheria yupo'na anatambulika kama ni Raia wa Nchi. Vilevile inawapa watu haki kama vile Elimu na kazi rasmi.***

Wazazi wameelezewa umuhimu wa watoto wao kua na hati na kuona hatua ya kutokomeza Umasikini uliopitiliza.

***"Huwezi kufanikiwa kama huna cheti cha kuzaliwa, ili utambulike kama ni Raia wa Tanzania." Mama Feisal***

Usajili wa vyeti vya kuzaliwa umefadhiliwa na Hilfe for Afrika na Kikundi cha Wanandoa wa Kidiplomasia (the Diplomatic Spouses Group).


POLYTANK
1000
14-1-2014
Hamisi hodari
Mimi napenda sana michezo. Jana ilikuwa siku ya michezo
shuleni kwetu. Wanafunzi wengi tulikusanyika.
Shule tatu zilishindana kucheza na kuimba.
Kabla ya michezo tuliondoa mawe na takataka Uwanjani.
Kiongozi wa michezo alisema watakaoshinda watapewa zawadi.
a e i o u
ba be bi bo bu
ga ge gi go gu
ha he hi ho hu
ja je ji jo ju
cha che chi cho chu
sha she shi sho shu
nda nde ndi ndo ndu
mba mbe mbi mbo mbu
nya nye nyi nyo nyu

*Upatikanaji wa Haki*

# Darasa la kufuta ujinga

***“Moja na njia ya kupambana na umaskini kithiri ni kufuta, ujinga kwa kuwa wezesha watu kujua, kusoma na kuandika.” Choloka***

***Tangu mwaka 2009 ATD dunia ya nne ilianzisha darasa la watu wasiojua kusoma na kuandika, darasa liliendelea Kundunchi katika mwaka 2014 kwa wakiwa wanafunzi 12.***

Wanachama wa ATD walisisitiza kufutaujnga ni hatua ya kutokomeza umaskini uiliokithiri: unaweza kuweka saini kwenye karatasi, kusafiri peke yako bila kutegemea mtu, kusoma magazeti n.k.

Mara mbili kwa wiki kwa kipindi cha miezi sita wanajami walijifunza kusoma na kuandika kwa pamoja na mwalimu. Mwenye taaluma katika sehemu iliotolewa na rafiki ATD. Walijifunza kusoma na kuandika kiswahili.

***Wakisaidiana kupata kufahamiana zaidi na lilikuwa darasa lenye maendeleo.***

Kidogo kidogo watu walisema wanajisikia kuweza na wana wezo wa kutetea haki zao, walifanya kazi kwa nguvu, kutokomeza hali ya kujisikia haibu katika ugumu wa kujifunza na kujivunia mafanikio nyao.

Bwana Kasiani, ambaye huwasaidia wanafunzi, alisema: “ ***...maisha yako yanabadilika. Kabla ya darasa, walitegemea kupata msaada kwa watu wengine. Baada ya kupata uhuru, wakati mwingine baadhi ya watu waliacha katika hatua ya awali kutokana na ugumu wake, lakini wanaweza kusudia tena darasa.***“


LIVE IN EXTREME POVERTY
TO ENSURE THAT THESE RIGHTS BE

# *Utamaduni*

**"Kabla ilinilazimu kulipia Ushonaji,**
**Sasa nasaidia Familia yangu**
**Na kuwaonyesha jinsi ya kufanya."**
**Mama Pendo**

## Ujuzi shirikishi: kugundua kupanda kwa pamoja

***Mwaka 2014 tulianzisha warsha ya ujuzi shirikishi. Baada ya mazungumzo na maandalizi ya muda, akina mama vijana wa Tandale waliamua kufanya kazi na kushirikiana katika Elimu, na Vipaji vyao.***

Wazo lao la kwanza lilikua ni kushirikiana katika Ujuzi wa kushona kwa pamoja. Kila Ijumaa jioni wanagundua vifaa, na hatua muhumu za kushona. Kidogo kidogo akina mama wanatengeneza vitu vyao vya mikononi, na kadhalika.

Kupitia warsha hiyo akina mama hujielezea kuhusu maisha yao, Nyumbani kwao, changamoto wanazo kumbana nazo na jinsi ya kuondokana na changamoto hizo.

***Ilikua sio swala la Ujuzi tu, pia kulikua na swala la Urafiki, Mshikamano na Ushirikiano.***

Asha, mama mmoja alisema: " ***sikufikiria kama nitakua na kipaji cha kushona,sasa naweza kutengeneza au kurekebisha nguo za watoto wangu, hata nguo za majirani zangu.kiukweli nimepata kujiamini.***"


ATD

# *Vijana*

> ***"Tunafurahi kuja kwenye lengo la kupambana na umaskini uliokithiri, ilikuleta mabadiliko katika jamii zetu, inanza na kutoka kwetu kuendelea kati familia"***
> ***Karama***

## Ujuzi shirikishi: kugundua kupanda kwa pamoja

***Katika kundi la vijana tuko vijana kutoka sehemu mbali mbali Dar es Salaam. Tuna kutana mara mbili kwa mwezi na tunaendesha maktaba ya mtaa jumamosi. Ndani ya jami yetu shuguli hii na inafanya wazee kuona kujitolea kwetu nzuri.***

Katika mkutano kila moja yuko huru kutoa mawazo kwa kuaminiana na kua kwetu pamoja kunatufanya kujenga urafiki ulio imara na kuleta matumaini. *"Najisikia niko na wenzangu pale tunapo jadili pamoja, tuna jisikia ni wa moja."*

***Mwaka jana tulishiriki siku ya kimataifa ya kuto komeza umaskini. Katika mwaka huo tulitembelea kituo cha jamii Kigamboni Community Center ilikuona namna gani makundi ya vijana waliyoanza na waliyofanikiwa.***

***"Kundi la vijana marafiki inatoa fursa kwa vijana kuja kufanya kitu kwa taifa letu" - Elizabeth***



# *Ushiriki*

***"Kwangu mimi ATD ni kama Familia yangu sio kama NGOs Nyingine, tunafanya maamuzi kwa pamoja.
Mikutano yetu hua ipo katika vielelezo vizuri."
Venance***

## Kundi la ushauri

***Kundi la ushauri la ATD ni mfano wa jinsi gani wanachama wa ATD wanafanya kazi kwa pamoja katika mambo yanayoleta Maendeleo ya harakati za ATD Tanzania na njia za kupigana dhidi ya Umasikini uliopitiliza.***

Kufanya kazi kwa ushirikiano, kusikiliza wazo la kila mtu, kuruhusu watu kujielezea, ili kufanya wajiamini zaidi, hiyo ni changamoto kubwa ambayo huonyesha kwamba inawezekana kwa jamii nzima.

***Kwasababu wanachama wa kundi wanautafauti*** mkubwa wanapotokea katika Uchumi,Jamii na Elimu, mawazo yanayopatikana yanakua na maana na Ufanisi.
Kundi hukutana mara moja kwa mwezi na kufanya kazi katika harakati za kimataifa za ATD, kuandaa matukio, kama vile siku ya kimataifa ya kutokomeza Umasikini, na kufanya tathmini ya kundiTangu lilipoanza mwaka 2009.



# *Matukio*

***"Mwaka 2014 nilikutana na watu sikufikiria kama nitakutana nao. Kupitia ATD nimeelewa kwamba kushirikiana na wengine ni muhimu kwangu kulikokufanya vitu peke yangu."***
***Yusuph***

## Siku ya kimataifa ya Kutokemeza Umasikini.

Kila mwaka, siku ya kimataifa ya kutokemeza Umasikini ni tukio ambalo huwawezesha watu wanaoishi katika Umasikini uliopitiliza kuongelea juu ya tabu wanazozipata na changamoto. Mandhari ya 2014 yalikua ni "usiache mtu nyuma: fikiri, Amua na fanya kazi ya kutokomeza Umasikini uliokithiri".

Kundi la ushauri lilipanga wapi, nani na wakati gani wa kusheherekea. Shule ya Buguruni ya watu wasiosikia [viziwi], Shule ya kujitolea kwa watoto wanaoteseka na Ubaguzi na Udhalilishaji.

***"Nilijisikia mwenye kujiamini na umuhimu wa wakati huu na watu waliokatika matatizo." - Kasian***

Siku iliandaliwa kwa kazi za kusafisha mazingira ya Shule kwa pamoja,kisha kupata taarifa kutoka kwa wanafunzi wa Buguruni na wanachama wa ATD.

Wanachama wa ATD waligundua namna gani watu wasio na uwezo [walemavu] ni lazima waishi na wenzao na si pembezoni mwa Jamii. Kati ya waalimu na wanafunzi waligundua Mshikamano.

***"Nilipigwa butwaa namna gani watoto walivyoishi na waalimu wao, karibu na njia ya ATD, huu ni wito wa kuweka nia." - Venance.***



# Familia

***"ATD hawakati tama ya kutembelea familia Tandale, na polepole wanachama wa ATD wataelewa kuhusu Umasikini."***
***Bibi Teddy***

## Kua karibu na familia

***Kitu cha kwanza kilichopewa kipaumbele na ATD ni kutafuta watu wanaoishi katika Umasikini uliokithiri. Njia ya kwanza ni kutembelea watu na kuelewa kiundani kuhusu masiha yao. Tunatengeneza uhusiano wenye uaminifu, kushirikiana wakati wa furaha, mafanikio na changamoto za kila siku.***

Baada ya mchakato mrefu, kwa muda huu kuna uwezekano wa kufanya sauti zao zisikike, uzoefu wao na uelewa wao mbele ya Jamii.

"***ATD itatuonyesha jinsi ya kuishi kwa pamoja, na jamii, na kutafuta ufumbuz***" ***- Mama Furaha***

**Kutembelea familia inatuwezesha sisi kuelewa matatizo yao na kutafuta njia ya kusaidia familia ambazo hazipeleki watoto wao shule. Kwa kutembelea familia mara kwa mara, inatengeneza uaminifu mkubwa, wanafamilia huelezea matatizo binafsi yanayowakumba bila kuona aibu.**

Kwa kutembelea nyumba za wanafamilia na sehemu zao za kazi, wanafamilia hutushukuru na huwasiliana na wanachama wote wa ATD Tanzania.

**"*Kuwakaribisha mara kwa mara watu kutoka ATD nyumbani kwangu, iliondoa upweke wangu, ilifumbua macho yangu na kunifanya niwe na fahamu, kwa mfano umuhimu wa Elimu.*" - *Mama Athumani.***


BARKA BOOKS
meijer reuse

# *Elimu*

***"ATD hufikiria kuhusu familia zinazoishi katika hali mbaya***
***Na hurahisisha zoezi la kwenda shule."***
***Mama Feisal***

## Upatikanaji wa shule

***Ni jukumu letu kuhakikisha kila haki ya binadamu inaheshimiwa. Kwenda shule ya msingi ni haki ya kila mtoto. Wazazi wanaoishi katika Umasikini wanahakikisha haki hii inaheshimika kwa ajili ya watoto wao. Wengi wamefanikiwa, lakini kwa baadhi, changamoto ni kubwa zaidi. Leo hii Tanzania watoto wengi hawahudhurii shule ya Msingi.***

Kupitia Shule watoto hujifunza namna ya kuishi na wenzao na kupata uwezo wa kujiamini zaidi. Inafungua nafasi ya kupata elimu ya juu zaidi, ujuzi na kazi.

**Mwaka uliopita ATD Dunia ya Nne ilisaidia watoto kama khamsini kupata haki yao ya shule ya msingi.**

Hii ni pamoja na kusaidia wazazi kupata vyeti vya watoto wao vya kuzaliwa na kuwaanzisha shule Januari2015; kusaidia wazazi kuandikisha watoto wao darasa la kwanza au Memkwa; na kusindikiza wazazi kukutana na walimu wakuu wa shule kama kulikua na kutokuelewana na watoto wakawawamerudishwa Nyumbani kutoka shule.


WE SHALL
HANGE TOGETHER.
shall

***Timu mpya ya ATD***

## Upatikanaji wa shule

*“Sisi ni kama familia moja”*

Kila mtu huleta mawazo yake, shauku, maarifa, ujuzi na ahadi katika vita dhidi ya Umasikini. Watu wanaoishi katika Umasikini uliokithiri, ni marafiki wa ATD, kila mwanachama wa ATD hutafuta njia ya kipekee kufanya kazi vizuri zaidi.

Kitu kinachotuunganisha ni kukataa kumuacha mtu nyuma wakati wengine wanaenda kukutana na wana familia. Tumeungana kwa imani moja.

Watu wa kujitolea hushiriki katika vita hii. Huchagua kuishi maisha ya kawaida, karibu na watu wanaoishi katika Umasikini uliokithiri. Huunga mkono wanachama na kuhakikisha malengo ya wanaharakati wa Tanzania yanafikiwa.

Kwa pamoja mwaka 2014 Hamisi, Hemed, Reachel and Robert, walijumuisha timu. Tokea mwisho wa mwaka timu imekua na leo 2015 tumekaribisha wanachama wengine Alexie, Cristal, Laurent, Leo, Salehe na Salma.

# ATD Dunia Ya Nne Tanzania
# Malengo kwa 2014 - 2017

***Utangulizi "Nitakuwa wapi kesho"***

Kutokuwa na sehemu maalum ya kuishi, hofu kila siku nitakula nini. Kudharauliwa na mbaya zaidi kuonekana hawana thamani, elimu duni watoto kutokwenda shule, hukumbwa na magonjwa mbali mbali, kufikiri kwamba kila wanachokifanya hakiwezekani. Haya ndio maisha ya watu maskini, hayana mwelekeo na huendelea kujiuliza ingawaje na juhudi zao zote, "*Nitakuwa wapi kesho?"*

*Japokuwa umaskini ni janga kubwa ni kama mtu alie fumbwa mdomo na kushindwa kuongea, Lakini ni watu ambao juhudi zao katika kuijenga dunia yenye amani na kuweza kuishi katika hali ya usawa na kutambulika kwa watu wengine.*

***Malengo***

**Thamani ya binaadamu wote ni sawa- kipaumbele kwa maskini**

Kipaumbele cha ATD Dunia ya Nne ni kwenda hatua kwa hatua, bega kwa bega, na watu maskini katika vitu vyote tunavyofanya. Ili kujenga uwaminifu, ushirikiano mzuri na kuifungua mioyo, akili zetu na kujuana vizuri na kuendelea kuwatafuta watu wengine wasiokuwepo. Tunapaswa kuheshimu na kuzingatia vikwazo wanavyokutana navyo kila siku na kuitia moyo jamii kujua juhudi na namna ya kujenga jamii nzuri..

## Kujifunza katika maisha

Ni ile shauku ya kujifunza kutoka kwa watu wanaoishi katika hali ya umaskini katika rika zote haiwezi kupungua. Ukiangalia maisha magumu wanayo kumbana nayo. Kiundani uelewa wetu ni juu ya sura nzima ya elimu na kujifunza maisha,huanzia nyumbani katikaka jamii, shuleni na kwa ujumla kwenye maeneo yanayotoa elimu. Kipaumbele kitakua kutambua zile juhudi wanazozifanya watu wanaoishi katika umasikini na vikwazo wanavyo kumbana navyo katika kufanikisha suala la ujuzi. Lazima kuwasisitizia kujifunza kwa furaha na kuwatia moyo kwa kushiriki katika mafunzo yao na si kwa kufanya mashindano.

## Vijana – ndio taifa la kesho

Katika kipindi cha ujana ni kipindi ambacho kila mmoja anataka kuonekana kuwa ni mtanashati na kujionyesha mbele za watu, lakini hukabiliwa na majukumu mazito ya kusaidia familia zao. Tutaendelea kuwatia moyo vijana kutoka matabaka tofauti kujitambua na kutimiza ndoto zao. Kuhakikisha kuwa juhudi zao zinatambulika katika jamii zao kama kujenga amani na kujenga taifa lao.

## Dunia ni ya wote

Harakati zetu, mtazamo wetu, ni kwa dunia, kwa maskini na matajiri, kwa binaadamu wote kuishi kwa amani, umoja, utu na njia nzuri ya maisha. Tutawawezesha watu kufahamu na kuzifikia haki zao za msingi. Katika kueneza ujumbe tutashirikiana mitazamo, kwa kuanza na majirani, jamii yetu na walio mbali. Tutadumisha mshikamano na kuunda urafiki baina ya watu na makundi na kupeana ufahamu, mawazo na ujuzi tulionao kwa manufaa ya wote.



**ATD Dunia ya Nne**
Imesajiliwa kwa namba 003447 chini ya sheria ya Asasi zisizo za kiserikali ya mwaka 2002
S.L.P. 61786, Dar es Salaam – Tanzania
atd.tanzania@gmail.com
Tovuti ya Kiingereza: www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html
Tovuti ya Kiswahili: www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html